JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA, BUNGE, URATIBU NA WENYE ULEMAVU




KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA
40412 DODOMA



JARIDA LA MTANDAONI • WWW.OWM.GO.TZ • NOVEMBA 2025






Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amuapisha Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma,



Makabidhiano ya Ofisi baina ya Waziri Mkuu Mstaafu Kassim Majaliwa na Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mlimwa Jijini Dodoma



# MAPOKEZI WA WAZIRI NA NAIBU WAZIRI



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu Mhe. Willium Lukuvi amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumuamini na kumrudisha kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Dkt. Jim Yonazi amewapongeza kwa uteuzi huo na kusema kuwa ofisi yake ipo tayari kufanya kazi kwa bidii, uaminifu na juhudi ili kuweza kutimiza malengo ya Mhe. Rais.










Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu Mhe. Ummy Nderiananga amekutana na kufanya mazungunzo na Wajumbe wa Bodi ya Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu Tanzania **(SHIVYAWATA)**.











Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) Mhe. Ummy Nderiananga amezindua rasmi mashindano ya Baiskeli ya Springhill Academy (SACRA 2025) ambayo yamefanyika katika barabara za Mtumba jijini Dodoma.

Mhe. Nderiananga amehimiza vijana kutumia mashindano na michezo hiyo kama sehemu ya kujenga ushirikiano, upendo na umoja kwa kila mtu bila kubagua hali walizonazo.









Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu Dkt, Jim Yonazi amesema ujenzi wa nyumba ya Mwanachi Mwenye Mahitaji Maalum Hanang Mkoani manyara umekamilika.

Dkt yonazi amepongeza uongozi wa Mkoa wa Manyara kwa usimamizi mzuri wa ujenzi wa nyumba hiyo, na hivyo ameelekeza uongozi wa Mkoa kumkabidhi Bi, Betrina Basili Fransis nyumba hiyo iliyojengwa Kijiji cha Waret wilaya ya Hanang Mkoani Manyara.





JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU



Pakua jarida hili kupitia:
www.pmo.go.tz

**Jarida hili hutolewa na:**

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu